

District scolaire **francophone Sud**
Apprendre. Grandir. Devenir.

1-833-533-3664 (TOLL FREE)

MPANGO KAMILI KWA AJILI YA KURUDI SHULE MWAKA 2020

Mpango kamili kwa ajili ya kurudi shule mwaka 2020 katika kipindi cha gonjwa-tandavu la COVID-19 umeandaliwa na Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto kwa kushirikiana na Afya ya Umma.
Kusudi la mpango huu ni kuzipatia shule na familia mwongozo kuhusu kurudi shule. Madhumuni ni **kupunguza uwezekano wa kuenea kwa COVID-19,** huku ukihakikisha upatikanaji wa elimu bora na huduma za wanafunzi. Mwongozo kwa wazazi na umma umechapishwa, na kila shule ina mpango kazi.

NANI ANAPASWA KURUDI SHULE?

Ujifunzaji kamili kwa wanafunzi wote utaanza watakaporudi shule mwaka 2020. Wanafunzi wa chekechea hadi Gredi la 8 watajifunza shuleni, huku wanafunzi wa sekondari ngazi ya juu watajifunza shuleni na nyumbani. Muda wa masomo utatofautiana kwa gredi na shule.

Madhumuni ya ujifunzaji yaliyowekwa kwenye mtaala ni **ya lazima katika kipindi cha mwaka wa masomo wa 2020-2021.** Walimu watawasaidia na kuwapima wanafunzi kwa mafanikio yao ya matokeo ya ujifunzaji.

IKIWA MTOTO WANGU YUPO HATARINI KWA SABABU ANA UGONJWA

- **Shauriana na daktari wako** ili kujua kama mtoto wako anapaswa kwenda shule ama la.

- **Kama mtoto wako hawezi kuhudhuria shule kwa sababu ya tatizo la afya la kimwili au kiakili,** mpango wa ujifunzaji utaandaliwa kwa ajili ya mtoto wako na mwalimu wake na mtaalamu wa usaidizi wa kielimu.

KABLA YA KUMPELEKA MTOTO WANGU SHULE

- ☑ Pima joto la mtoto wako kabla hajatoka kwenda shule.

- ☑ Kama mtoto wako ana dalili za COVID-19, **unapaswa kumbakiza mtoto wako nyumbani na kupiga 811.**

- ☑ Ikiwa mtoto wako ni mzima na hana dalili, **unaweza kumpeleka mtoto shuleni.**

- ☑ **Hakikisha mtoto wako ana barakoa iliyosafi ya kwenda nayo shule.**

- ☑ Mtoto aliye mgonjwa au mtu mwenye dalili za COVID-19 **hawezi kurudi shule hadi awe amepona kabisa.** Afya ya Umma itakujulisha ni lini kipindi cha kujitenga na watu wengine kitakoma.

Mtoto au mtu mwenye mzio wa msimu au anasumbuliwa na mafua sugu au ana makamasi anaruhusiwa kurudi shule.



District scolaire **francophone Sud**
Apprendre. Grandir. Devenir.

1-833-533-3664 (TOLL FREE)





JE, USAFIRI WA SHULE UTATOLEWAJE WAKATI SHULE ITAKAPOANZA?

Inawezekana kutakuwa na **mabadiliko ya njia na ratiba za usafiri wa shule** ili kuwezesha suala la kujitenga na kuzuia wanafunzi kukusanyika katika eneo moja na kwa wakati mmoja.

M>5 **Mwanafunzi mmoja au wawili wa familia moja** kwa kila kiti ili kuzingatia suala la kujitenga na watu wengine pale barakoa zisipovaliwa.

6>12 **Mwanafunzi mmoja au wawili wa familia moja wakiwa wamevaa barakoa** pale wanapopanda na kushuka kwenye basi. Wanafunzi wanaweza kuvua barakoa zao kama wakakaa peke yao au na mwanafamilia mwenzake.



Pale suala la kujitenga na watu wengine linaposhindikana, **wanafunzi wanapaswa kuvaa barakoa.**

Huduma za usafiri wa shule zinarekebishwa ili kuhakikisha uzingatiaji wa hatua hizi.



NANI ANAWEZA KUINGIA SHULENI?

- **Wanafunzi na wafanyakazi wa shule** wanafasiliwa kwenye *Sheria ya Elimu* (walimu watembeleaji, wafanyakazi wa wilaya, wajitoleaji, na rasilimali watu wengine).
- Walimu watembeleaji na wafanyakazi wa shule wanaofanya kazi katika zaidi ya shule moja, **watalazimika kufuata utaratibu wa ziada.** Wilaya ya shule itajaribu kupunguza idaidi ya shule zinazotembelewa na wafanyakazi hawa.
- **Mtu yeyote aliyeidhinishwa na mkuu wa shule** (matengenezo, dharura, wafanyakazi wa masuala ya kijamii, nk.).
- **Wakaguzi fulani,** kama vile wawakilishi wa WorksafeNB na Afya ya Umma, **wanaweza kufanya ukaguzi maalum.**
- **Matumizi ya kijumuiya ya shule yamesitishwa hadi itakapotangazwa vinginevyo.**
- **Vikao vya vikundi na matukio mengine makubwa ya shule yatafanyika mtandaoni.**


NAWEZA KUMTEMBELEA MTOTO WANGU SHULENI?

- Ziara za kustukiza au zisizo na miadi zitakuwa **chache na hazitahimizwa kabisa.**
- **Mawasiliano kwa njia ya mtandao au kwa simu itakuwa ndiyo njia kuu ya mawasiliano.** Kama kikao ana kwa ana kitakuwa lazima, kinapaswa kuzingatia miongozo ya afya na usalama. **Mpango kazi wa shule unaweza kuhitaji barakoa zivaliwe.**



District scolaire **francophone Sud**
Apprendre. Grandir. Devenir.

1-833-533-3664 (TOLL FREE)



UJIFUNZAJI UTAFANYIKAJE WAKATI WA GONJWA-TANDAVU HILI?

Madhumuni yaliyopangwa ya ujifunzaji yatakuwa ya **lazima kwa mwaka wa shule wa 2020-2021.** Mtaala utahakikisha kwamba matokeo muhimu yanafikiwa.

Maeneo yote yaliyopo ambayo yanawezesha ujifunzaji na maisha ya shule yatatumika ili kuunga mkono ujifunzaji (maeneo ya nje, maeneo ya jumuiya, maeneo ya nyumbani, nk.).

- **Inawezekana kwamba madarasa au makundi ya wanafunzi wa gredi tofauti yataungwanishwa.**
- **Upangaji upya wa maeneo** ya pamoja ili kuhakikisha kujitenga kati ya makundi ya wanafunzi lakini pia kati ya wanafunzi na watu wazima.
- **Ratiba kubadilishwa ili kupunguza msongamano ndani na nje ya shule** na kuhakikisha uwekaji makundi ya wanafunzi au suala la kujitenga (mapumziko, chakula cha mchana, kuchukuliwa na kuletwa kwa wanafunzi, na safari nyingine).



Vifaa vinavyotumiwa na wanafunzi mbalimbali (kompyuta, vifaa vya kielektroniki, vifaa vya michezo, ala za muziki, nk.) **vitasafishwa na kutakaswa baada ya kila matumizi na mfanyakazi wa shule.**

- **Kama haiwezekani kusafisha na kutakasa kifaa, kinapaswa kutumiwa na mwanafunzi mmoja tu au kutotumiwa kabisa.**

SHUGHULI ZITAFANYIKAJE?

- Shughuli binafsi au zinazohitaji eneo zaidi kati ya wanafunzi na wafanyakazi wa shule ili kuwezesha kujitenga na watu wengine.
- **Chekechea hadi Gredi la 8:** Wanafunzi wanawekwa katika makundi ya wanafunzi (bubbles). Kujitenga na watu wengine si lazima kwa makundi haya.
- **Sekondari Ngazi ya Juu:** Wanafunzi wanapaswa kudumisha kujitenga kwa mita 1 darasani, mita 2 nje ya darasa au mita 1 wakivaa barakoa.
- **Timu za elimu katika wilaya za shule na Idara zimefanya kazi ya kujua namna ujifunzaji utakavyopewa kipaumbele ikiwa kuondoka katika awamu moja kwemda nyingine kutaathiri mtiririko wa ujifunzaji au utoaji wa elimu.**

  Kujifunza itakuwa lazima, na maendeleo ya wanafunzi yatapimwa.

Wanafunzi wa Gredi la 9 hadi la 12 ***watatumia mifumo mbalimbali ya kidijitali kwa ajili ya kazi zao za ushirikiano*** *na ujifunzaji wao, wa shuleni na wa masafa, watakaporudi shule mwaka 2020.*


Programu ya BYOD (Bring Your Own Device) *iliyoanzishwa na Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto (EECD)* ***inawahimiza kuja shuleni na vifaa vyao vya kiteknolojia.*** *Familia zenye ustahili zinaweza* ***kuwasilisha maombi kupitia portal ya mtandaoni kwa ajili ya wazazi.*** *Taarifa zaidi kuhusu programu ya BYOD itatumwa moja kwa moja kwa familia, ambazo zinaweza pia kupiga* **1-833-533-3664 (TOLL FREE).**





District scolaire **francophone Sud**
Apprendre. Grandir. Devenir.

1-833-533-3664 (TOLL FREE)



USAFI WA KIMWILI SHULENI?

Matumizi ya vitakasaji vilivyothibitishwa nchini Canada.

Kuwapa mafunzo wafanyakazi jinsi ya kutumia bidhaa hizi.

Kusafisha na kutakasa viambaza na vitu vinavyoguswa sana (vitasa, vishikio vya ngazi, nyenzo za kielimu, nk.) angalau mara mbili kwa siku na pale vinapokuwa si visafi.

Vitu ambavyo wanafunzi wanaviweka mdomoni **vinapaswa kusuuzwa kwa maji baada ya kusafishwa na kutakaswa.**

Kutakuwa na kituo kimoja au zaidi cha kutakasa mikono kwa kila eneo la pamoja kulingana na ukubwa wa eneo husika.

WAKATI GANI MIKONO INAPASWA KUOSHWA?

Ili kuzuia virusi hivi kuenea, wafanyakazi wa shule na wanafunzi wanapaswa kunawa mikono yao kwa sabuni na maji mara kwa mara.

Wafanyakazi wa shule sharti wanawe mikono yao katika hali zifuatazo:
- kabla na baada ya kushika chakula
- baada ya kumsaidia mtoto kutumia choo
- baada ya mapumziko
- kabla na baada ya kutoa dawa.

TABIA HUSIKA UWAPO SHULENI

- Epuka **salamu za kukaribiana** (k.m., kukumbatiana na kushikana mikono).
- Wanafunzi wa Gredi la 6 hadi la 12 **wanapaswa kutakasa madawati na viti vyao baada ya kila somo.**
- Idadi ya wanafunzi **wanaokwenda chooni kwa wakati mmoja** inapaswa kuwa ndogo.
- **Wafanyakazi wa shule wanapaswa kudumisha kujitenga kwa mita mbili wao kwa wao.**
- Makundi ya wanafunzi (bubbles) yanapaswa kudumisha kujitenga kwa mita mbili (2) na makundi mengine. Nje ya makundi hayo, wanafunzi wanapaswa kudumisha kujitenga na watu wengine kwa mita mbili (2) au moja (1) kama wamevaa barakoa.
- Wafanyakazi wa shule wanapaswa kuhakikisha kwamba wanafunzi wananawa mikono yao kabla na baada ya mapumziko.
- Mabomba ya bubujiko la maji hayatatumika. Unapotumia kituo cha kujaza maji, **hakikisha chupa yako haigusani na bomba la maji.**
- Epuka kugusa uso, macho, pua na mdomo wako.
- Kohoa na piga chafya kwenye kiwiko chako au ziba mdomo na pua yako kwa kutumia tishu ya matumizi ya mara moja. **Tupa mara moja tishu zilizotumika, na nawa au takasa mikono yako.**
- **Wanafunzi na wafanyakazi wa shule sharti wanawe mikono yao katika hali zifuatazo:**
  - wanapowasili shuleni (utakasaji unakubalika)
  - kabla na baada ya chakula
  - baada ya kutumia choo
  - baada ya kupenga pua zao au kukohoa au kupiga chafya
  - baada ya kutumia vichezeo, kitu cha pamoja, au nyenzo ya ujifunzaji
  - kabla na baada ya kunywa dawa
  - baada ya kucheza nje



District scolaire **francophone Sud**
Apprendre. Grandir. Devenir.

1-833-533-3664 (TOLL FREE)



JINSI YA KUNAWA MIKONO YAKO KWA USAHIHI KWA SABUNI NA MAJI



Loanisha mikono



Tumia sabuni ya maji au mche ulio safi wa sabuni



Sugua mikono kwa nguvu



Hakikisha unaosha vizuri sehemu ya ngozi




Weka mkazo kwenye maeneo yanayozunguka kucha zako na katikati ya vidole vyako



Endelea kusugua mikono pamoja angalau kwa sekunde 20



Suuza na kausha mikono kwa usahihi



Ikiwezekana, tumia tishu kufunga bomba. Tumia tishu kufungua mlango na kisha itupe

Kama hakuna sabuni na maji na hakuna uchafu unaoonekana mikononi, tumia kitakasaji chenye alkoholi kilichothibitishwa na Health Canada. **Wanafunzi wadogo sharti wasimamiwe wanapotumia vitakasa mikono.**



Weka kitakasa mikono



Sugua nyuma na mbele ya mikono na kati ya vidole, maeneo yanayozunguka kucha, na kwenye viganja



Sugua mikono kwa nguvu



Endelea kusugua hadi mikono iwe mikavu

UVAAJI WA BARAKOA

- Wanafunzi wa Gredi la 6 hadi la 12 **watatakiwa kuvaa barakoa nje ya darasa.** Matumizi ya barakoa **nje ya darasa yanapendekezwa kwa wanafunzi wa chekechea hadi Gredi la 5.** Kuvaa barakoa darasani si lazima.
- Inapendekezwa kuvaa barakoa iliyo safi. Uvaaji wa barakoa unapaswa kuendana na kazi husika, na barakoa zinapaswa kuvaliwa na kutupwa au kufuliwa kwa usahihi. **Hazipaswi kuvaliwa kwa vipindi virefu vya muda.**
- Watu wanaovaa barakoa ambazo si za kitiba au kitu kinachofunika uso **wanaweza kupunguza kuenea kwa virusi kama kimevaliwa kwa usahihi.**
- Uvaaji wa barakoa peke **yake hautazuia kuenea kwa COVID-19. Unapaswa kuzingatia tahadhari za usafi wa kimwili na kudumisha kujitenga na watu wengine wakati wote.**